Jibu: Jibu la swali hili tutalipata katika ule mstari wa 22, sura ya 7 ya kitabu cha Mwanzo…

> *Mwanzo 7:22 "kila kitu chenye pumzi ya roho ya uhai puani mwake kikafa, kila kilichokuwako katika nchi kavu".*

Hapo yanatajwa mambo mawili,

1. Kila chenye roho ya uhai puani kikafa.

Kufuatia andiko hili, ni wazi kuwa samaki hawapumui kupitia pua kwasababu wao wapo chini ya maji..

2. Pia Kila kilichokuwako katika nchi kavu.

Kupitia maneno haya ni wazi kuwa gharika haikuwahusu viumbe wa majini au baharini, kwasababu hao hawaishi nchi kavu.

Vile vile hatusomi popote kuwa Nuhu aliingiza nyangumi, au kambale ndani ya safina, badala yake tunaona ni wanyama tu

peke yao, na tena walimfuata Nuhu mwenyewe na wala Nuhu hakwenda kuwatafuta, sasa kwa mantiki hiyo nyangumi wangemfuataje Nuhu safinani?.

Kwahiyo ni wazi kuwa gharika ile ilihusu viumbe waliooishi nchi kavu, ambao ni wanadamu ndege, wanyama na wadudu.

> *Mwanzo 7:20 “Maji yakapata nguvu, hata ikafunikwa milima kiasi cha mikono kumi na mitano.*
>
> *21 Wakafa wote wenye mwili waendao juu ya nchi, na ndege, na wanyama wa kufugwa, na kila mnyama wa mwitu, na kila kitambaacho chenye kutambaa juu ya nchi, na kila mwanadamu”*

Sasa kama ni hivyo, basi samaki walihifadhiwa wapi wakati wa gharika?

Jibu ni kwamba samaki waliendelea kubaki majini wakati wa gharika.

Lakini pamoja na hayo biblia inatabiri ujio wa gharika nyingine ambayo si ya maji tena bali ya moto, ambapo viumbe vyote vitafumuliwa na hakuna kitakachosalia..

> *2 Petro 3:6 “kwa hayo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji, ikaangamia.*
>
> *7 Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu.*
>
> *8 Lakini, wapenzi, msilisahau neno hili, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja.*
>
> *9 Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba.*
>
> *10 Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea.*

> *11 Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa".*

Bwana atusaidie tukae katika mwenendo wa UTAKATIFU na UTAUWA.

Maran atha.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >> https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Je gharika ya Nuhu iliangamiza hadi samaki wa baharini na nyangumi?.

Mafundisho mengine:

NAYE AKASIMAMA JUU YA MCHANGA WA BAHARI.

NUHU WA SASA.

UNAMCHUKULIA YESU KWAKO KAMA NANI?

KWANINI NI NUHU, AYUBU NA DANIELI?

Makasia ni nini? (Yona 1:13).

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp